


Silaha za Mungu

Pigana vita vya kiroho!



Waefeso 6:10-18

(10) Hatimaye, nawatakeni muwe imara katika kuungana na Bwana na kwa msaada wa nguvu yake kuu. (11) Vaeni silaha anazowapeni Mungu mpate kuzipinga mbinu mbaya za Ibilisi. (12) Maana yita vyenu si vita kati yetu na binadamu, bali ni vita dhidi ya jeshi ovu la ulimwengu wa roho; tunapigana na watawala, wakuu na wenye nguvu wanaomiliki ulimwengu huu wa giza. (13) Kwa sababu hiyo, vaeni silaha za Mungu ili siku ile itakapofika muweze kuyapinga mashambulio ya adui; na mkisha pigana mpaka mwisho, muwe bado thabiti. (14) Basi, simameni imara! Ukweli uwe kama **ukanda kinuoni** mwenu, uadilifu uwe kama **vazi la kujikinga kifuani**, (15) na hamu ya kutangaza. Habari Njema ya amani iwe kama **viatu miguuni** mwenu. (16) Zaidi ya hayo yote, imani iwe daima kama **ngao mikononi** mwenu, iwawezeshe kuizima mishale ya moto ya yule Mwovu. (17) Upokeeni wokovu kama **kofia yenu ya chuma**, na neno la Mungu kama **upanga mnaopewa** na Roho Mtakatifu. (18) Salini daima, mkiomba msaada wa Mungu. Salini kila wakati kwa nguvu ya Roho. Kesheni bila kuchoka mkisali kwa ajili ya watu wote wa Mungu.

Biblia inasema

Silaha za Mungu:

Warumi 13: 12

Tusiwe na ulafi na ulevi, uchafu na uasherati, ugomvi na wivu.

Zekaria 4: 6

Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema BWANA wa majeshi.

Biblia inasema

Pigana vita vya kiroho:

Warumi 15: 30

Basi, ndugu zangu, nawasahi kwa kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristo, na kwa ajili ya upendo ulietwao na Roho, mniunge mkono kwa kuniombea kwa Mungu.

Zekaria 4: 6

Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema BWANA wa majeshi.

Biblia inasema

Kutumikia na Mungu:

Wakorintho 6 : 3-10

³Kusudi tusiwe na lawama yoyote katika utumishi wetu, hatupendi kumwekea mtu yeyote kizuio chochote. ⁴Badala yake, tunajionyesha kuwa kweli watumishi wa Mungu kwa kila kitu: kwa uvumilivu mwingi wakati wa mateso, shida na taabu. ⁵Tumepigwa, tumetiwa gerezani na kuzomewa hadharani; tumefanya kazi tukachoka; tumekesha na kukaa bila kula.

⁶Tunajionyesha kuwa watumishi wa Mungu kwa usafi wa moyo, elimu, uvumilivu na wema; kwa Roho Mtakatifu, kwa upendo usio na unafiki, ⁷kwa ujumbe wa kweli na kwa nguvu ya Mungu. Uadilifu ndiyo silaha yetu upande wa kulia na upande wa kushoto. ⁸Tuko tayari kupata heshima na kudharauliwa, kulaumiwa na kusifiwa. Twadhaniwa kuwa waongo, kumbe twasema kweli; ⁹kama wasiojulikana, kumbe twajulikana kwa wote, kama waliokufa, lakini mwonavyo, sisi ni wazima kabisa. ¹⁰Ingawa tumeadhibiwa, hatukuuawa; ingawa tunayo huzuni, twafurahi daima; ingawa tu maskini hohehahe, lakini twatajirisha watu wengi; twaonekana kuwa watu tusio na chochote, kumbe tuna kila kitu.

Biblia inasema

Lengo:

1 Yohane 5: 4-5

Hivi ndivyo tunavyoshinda ulimwengu: kwa imani yetu. Nani, basi, awezaye kuushinda ulimwengu? Ni yule anayeamini kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu.

